Januari 2021

# Athari za janga la CORONA katika Sekta isiyo rasmi: Wafanyakazi wa Sekta Isiyo Rasmi Dar es Salaam, Tanzania



*Ashura Abdallah ni mfanyakazi wa majumbani mwenye umri wa miaka 40 ambaye anategemewa na watoto. Picha na: Fanuel Halelwa.*

## Matokeo muhimu

1. Kabla ya janga hilo kuikumba Tanzania, wafanyakazi wa majumbani walikuwa wakifanya kazi, kwa wastani, wa siku 6.1 kwa wiki.
2. Kwa sababu ya kutokuwepo kwa zuio rasmi au la pamoja, 84% ya wafanyakazi wa majumbani Dar es Salaam waliweza kuendelea kufanya kazi mnamo mwezi Aprili.
3. Kati ya wale waliopoteza kazi zao kutokana na janga hilo, ni 11% tu ndio walilipwa na waajiri wao kwa kipindi ambacho hawakufanya kazi.
4. Hata kwa wafanyakazi wote wa majumbani wanaoishi na waajiri wao, 27% waliripoti kufanya kazi masaa mengi kuliko hapo awali.
5. 12% ya wafanyakazi wa majumbani waliripoti visa vya njaa katika kaya zao (zinazoathiri watoto au watu wazima), lakini kiwango hiki kinaongezeka hadi 47% kati ya wafanyakazi walioacha kufanya kazi mnamo Aprili.
6. Ili kukabiliana na athari za janga hilo, asilimia 54 ya wafanyakazi wa majumbani walitumia mikakati mbalimbali kama vile kukopa pesa, kutumia akiba au kutafuta msaada kutoka kwa familia, marafiki au majirani.

## Utangulizi

Janga la COVID-19 katika Sekta isiyo o Rasmi ni utafiti unaoongozwa na WIEGO kwa miji 12 unaotathmini athari za janga la COVID-19 kwa vikundi maalum vya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi na kaya zao. Kwa kutumia dodoso la uchunguzi na mahojiano ya kina, Raundi ya 1 ilitathmini athari za janga mnamo Aprili 2020 (kipindi cha zuio katika miji mingi) na mnamo Julai 2020 (wakati utafiti ulifanywa na vizuizi vilipunguzwa katika miji mingi)[1] ikilinganishwa na Februari 2020 (kabla ya COVID-19). Kipindi cha 2 kitakagua athari zinazoendelea dhidi ya ishara za kupona mnamo Machi-Aprili 2021, ikilinganishwa na kipindi cha kabla ya COVID-19 na Kipindi cha 1. Ripoti hii inawasilisha muhtasari wa matokeo ya Kipindi cha kwanza cha utafiti Jijini Dar es Salaam, Tanzania. Watafiti jijini Dar es Salaam walichunguza wafanyakazi wa Majumbani 283 ambao ni wanachama wa chama cha Wafanyakazi wa Hifadhi, Hoteli, Majumbani, Huduma za Jamii na Ushauri (CHODAWU). Walihoji pia viongozi wawili wa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi na watoa taarifa wawili muhimu kutoka kwa mashirika ya wanachama.

Utafiti hutoa wasifu wa wafanyakazi, unaeleza hali zao za kazi na athari za COVID-19. Wakati Tanzania haikutekeleza zuio la kutoka ndani, utafiti unaonyesha kuwa hali za wafanyakazi wa majumbani tayari zilikuwa mbaya hata kabla ya janga la COVID 19.




[1] Katika kipindi cha Juni /Julai wakati utafiti ukifanywa ilikuwa "siku saba za mwisho" kabla ya mahojiano ya utafiti.

## Sekta isiyo rasmi Dar es Salaam


Karibu robo tatu (76%) ya wafanyakazi wasio wa kilimo wa Tanzania wameajiriwa katika sekta isiyo rasmi. Ndani ya Dar es Salaam, kiwango cha sekta isiyo rasmi hufikia 58% (ILFS, 2014).[1]


Kati ya idadi ya watu wenye umri wa kufanya kazi, 5% wameajiriwa kama wafanyakazi wa majumbani, kulingana na utafiti wa ILO. Ingawa, takwimu hii inaweza kua imeshushwa na iko karibu na 7% kwa sababu miongoni mwa mambo mengine, ajira za watoto chini ya umri wa miaka 15, kuenea kwa mipango isiyo rasmi, na kusita kwa wafanyakazi wa majumbani kujitambua kama vile kutokana na kuenea kwa unyanyapaa katika kijamii (ILO, 2014).

Tanzania bado haijaridhia Mkataba wa ILO namba 189, ambao unawalinda wafanyakazi wa majumbani, na wakati kuna kanuni za ajira za nchi ambazo zinaweka viwango vya chini vya mishahara na masharti mengine ya ajira, lakini utekelezaji bado ni mdogo.

## Ukubwa wa Sampuli na Muundo[2]

**Wafanyakazi wa majumbani 283**




* Mhojiwa mmoja hakuripoti jinsia.

**Hali ya uhamiaji:**
Asilimia 10 ya wafanyakazi wa majumbani waliofanyiwa utafiti wanatoka miji mingine nchini Tanzania.

**Hadhi ya ajira:**
27% ya wafanyakazi wa majumbani waliofanyiwa utafiti waliishi katika makazi ya mwajiri wao.

**Wastani wa siku za kazi:**
Kabla ya janga, wafanyakazi wa majumbani walifanya kazi kwa wastani wa siku 6.1 kwa wiki. Ingawa sheria ya nchi inaweka siku sita za kufanya kazi kwa wiki, 25% ya wafanyakazi waliochunguzwa walifanya kazi siku 7.

**Mapato:**
Mishahara ya wafanyakazi wa majumbani inasimamiwa na sheria ya nchi na hutofautiana kulingana na kazi ya mwajiri. Kwa nadharia, malipo ya kila mwezi yanaweza kuwa kati ya TZS40,000 na TZS250,000, lakini utafiti wetu unaonyesha kwamba 2% ya wahojiwa walikuwa chini ya kiwango hiki cha kisheria na 1% walikuwa juu ya kiwango.

| | Wastani | Kati |
|---|---|---|
| Wastani wa mapato ya kila siku ya wahojiwa mnamo Februari (kabla ya COVID-19) | TZS4,837 | TZS4,792 |

- Utafiti ulifanywa mnamo Julai 2020.
- Mahojiano yaliyopangwa nusu yalifanywa mnamo Agosti na Septemba 2020.

2 Sekta isiyo rasmi haijumuishi kila aina ya shughuli za kilimo, ambazo zinachangia asilimia 66 ya wafanyakazi walioajiriwa nchini Tanzania.

3 Sampuli ya utafiti ni uwakilishi wa wanachama wa CHODAWU kuliko idadi ya wafanyakazi wa majumbani nchini Tanzania. Kulingana na utafiti wa ILO mnamo 2016, asilimia 75 ya watu wanaofanya kazi za majumbani nchini Tanzania ni wanawake; 68% hufanya kazi katika wilaya nje ya mahali pa asili; na 78% ya wafanyakazi wa majumbani ni kati ya miaka 15 hadi 24. Utafiti wetu unaonyesha sampuli ya zamani, na uwakilishi mdogo wa wanaume na wahamiaji (wa ndani na wa kimataifa).





*Digna Nicholaus ni mfanyakazi wa majumbani mwenye umri wa miaka 32 ambaye anategemewa na wazazi pamoja na ndugu. Picha na: Fanuel Halelwa.*

# Muda wa COVID-19 na Muktadha

Janga la COVID-19 lilifika Tanzania katikati ya mwezi Machi. Serikali ililenga kuweka uchumi uendelee na kuepukana na kufungwa kwa jumla. Hapo awali ilianzisha hatua kadhaa za kuzuia, lakini kufikia Juni nchi ilitangazwa kutokua na COVID-19- na vizuizi vyote viliondolewa.

## Nyakati



*"Kwa wakati huu, labda wengine watapoteza kazi na wengine wamelazimika kuondoka jijini, na wengine wanakabiliwa na ugumu wa mishahara midogo. Hili ni jambo ambalo unapaswa kuishi nalo. Baadhi yao walipata mfadhaiko wa akili kwa sababu ya mvutano na mawazo mengi. Itachukua muda kwao kupata nafuu. "*

**- Kiongozi wa Wafanyakazi wa Nyumbani**

# Athari na Majibu ya janga.

Athari kuu za janga hilo zilipunguza siku za kazi, mapato na chakula; kuongezeka kwa wasiwasi wa afya na usalama; na kuongezeka kwa majukumu ya kaya kwa wale wafanyakazi wa majumbani wanaoishi na waajiri wao.

## Kazi, Mapato na Chakula

Licha ya juhudi za serikali kuendeleza uchumi, kufungwa kwa hoteli mwishoni mwa Machi, Aprili na Mei, na kupunguzwa kwa jumla kwa sekta zinazohusiana na wageni (utalii, usafirishaji, kilimo cha maua) kulikuwa na athari mbaya kwa uchumi zinazoathiri viwandani na mwishowe kupunguza mahitaji ya ndani. Katika mlolongo huu, wafanyakazi wa wajumbani walipoteza kazi, ucheleweshwaji wa mishahara na mizunguko ya kazi isiyo ya kawaida. Ingawa imeenea sana kuliko miji mingine, ukosefu wa ajira jijini Dar es Salaam ulisababisha kupunguzwa kwa mishahara na ukosefu wa chakula kwa baadhi ya kaya.

## Athari kwa Kazi

Hatua za kuzuia maambukizi nchini Tanzania hazikuwa kali sana kama nchi za jirani. Kwa sababu ya kutokuwepo kwa zuio la kufungiwa ndani kwa jumla, wafanyakazi wengi wa majumbani Dar es Salaam waliweza kuendelea kufanya kazi katika miezi ya kwanza ya janga hilo. Mnamo Aprili, wakati kisa cha mwisho kiliporipotiwa, asilimia 84 ya wafanyakazi wa majumbani waliofanyiwa uchunguzi walikuwa bado wanafanya kazi.

Miongoni mwa wale ambao waliacha kufanya kazi (16% au wafanyakazi wa majumbani 45), sababu kuu ilikuwa waajiri wao kuwasimamisha kazi kwa sababu ya wasiwasi wa afya zao au kwa sababu hawakuweza kumudu mishahara yao, kulingana na mahojiano. Kufikia Julai, 87% (au 244) ya wafanyakazi wa majumbani walikuwa wakifanya kazi.


Athari katika kazi pia inaweza kuonekana katika kupunguzwa kwa siku za kazi. Mnamo Februari, kabla ya janga hilo, wafanyakazi wa majumbani Dar es Salaam walifanya kazi kwa wastani wa siku 6.1 kwa wiki.

Wakati janga hilo halikuathiri uwezo wa kufanya kazi kwa walio wengi, wafanyakazi wengi ambao waliacha kufanya kazi mnamo Aprili hawakuanza tena kurudi kazini baadaye. Kufikia Julai, wafanyakazi hawa walikuwa wakifanya kazi, kwa wastani wa theluthi moja ya wakati ambao walikuwa wakifanya kazi kabla ya janga. Kwa kuongezea, ni 11% tu ndio waliolipwa na wajaari wao kwa wakati ambao hawakuweza kufanya kazi.

Mazingira ya kazi pia yailizorota kwa wale ambao waliendelea kufanya kazi, na hutofautiana kati ya wafanyakazi wa nyumbani wanaoishi na waajiri wao na wafanyakazi wanaoenda na kurudi. Wafanyakazi wote wanaoishi na waajiri wao (27% ya wafanyakazi wote wa majumbani waliohojiwa) waliweza kulinda ajira zao katika kipindi hiki chote, lakini hali zao za ajira zilizorota (rejea sehemu juu ya mafadhaiko wa kaya).

Wafanyakazi wa majumbani wasioishi na waajiri wao ilikuwa rahisi kupoteza ajira katika kipindi hiki, na wengi walitaja changamoto za usafiri (kuongezeka kwa gharama na upatikanaji wa usafiri) kama kikwazo kikuu. Kwa kuongezea, baadhi walilazimika kuhamia kwa waajiri wao na kutengana na familia zao.


**% ya wafanyakazi ambao waliendelea kufanya kazi**





*Mwanahamisi Hassan ni mfanyakazi wa majumbani mwenye umri wa miaka 22 ambaye anategemewa na wazazi. Picha na: Fanuel Halelwa.*

**Wastani wa siku za kufanya kazi katika wiki ya kawaida**






*"Kwa kipindi hiki, bosi anakwambia hana pesa, kwa hivyo lazima usubiri kulipwa mshahara wako."*

**- Mfanyakazi wa majumbani Mwanamke**

*"Kilikua kipindi kirefu mbali na watoto kwa sababu ilibidi nihamie kwa mwajiri wangu na kuiacha familia yangu nyumbani. Malengo yangu yote wakati huo yalisimama."*

**- Mfanyakazi wa majumbani Mwanamke**

### Athari kwa mapato

Kupunguzwa kwa siku za kufanya kazi kulileta athari kwa mapato, hasa kati ya wale ambao walipoteza uwezo wao wa kufanya kazi. Mnamo mwezi Aprili, wahojiwa walikuwa wamepoteza kwa wastani robo moja (26%) ya mapato yao ya kila siku ya Februari, na kufikia Julai mapato yao hayakuwa yamerudi katika viwango vya kabla ya janga.

Mtikisiko huu wa mapato unaelezewa zaidi na wahojiwa namba 61 na 51 ambao waliripoti mapato ya sifuri mnamo Aprili na Julai.

**Wastani wa mapato ya kila siku**






*"Ni katika hali hii tu ndio bosi anapata shida kukulipa; anasema uchumi umezorota".*

**- Mwanamke Mfanyakazi wa majumbani**


*"Wafanyakazi wa majumbani ni masikini, lakini kwa COVID-19 ilikuwa sababu ya nyongeza. Yeye ni masikini, mshahara ni mdogo sana, halafu wanafukuzwa au wanapata mshahara nusu. Ilikuwa ngumu ".*

**–Vicky Kanyoka, mratibu wa IDWF Kanda ya Afrika**

### Athari kwa chakula

Pamoja na kuripoti mapato yaliyopungua, asilimia 12 ya kaya zote ziliripoti visa vya njaa kwa watu wazima au watoto katika kipindi cha mwezi Mei. Kulingana na mahojiano, mwelekeo huu unaweza kuelezewa kutokana na kuongezeka kwa gharama za chakula na ukweli kwamba watoto sasa walikuwa wakikaa nyumbani kwa sababu ya kufungwa kwa shule. Matukio ya njaa yalikuwa ya juu kwa wale waliopoteza kazi zao mnamo Aprili: 47% (kati ya 43) waliripoti visa vya njaa, ikilinganishwa na 5% (kati ya 217) ya walioendelea kufanya kazi.

**Asilimia**
**47%**
**waliripoti visa vya njaa**
(Wahojiwa ambao waliacha kufanya kazi mnamo mwezi Aprili)



**Asilimia**
**5%**
**waliripoti visa vya njaa**
(Wahojiwa ambao waliendelea kufanya kazi katika kipindi cha mwezi Aprili)





*"Moja ya athari za COVID-19 ilikuwa kulala na njaa." - Mfanyakazi wa majumbani Mwanamke*

---

[4] "Matukio ya njaa" yanajumuisha makundi yote ya wahojiwa wote ambao waliripoti kuwa huenda watu wazima (miaka 16 na zaidi) au watoto katika kaya walikumbwa na njaa (mara zote, mara nyingi, wakati mwingine, mara chache).


[5] 16% (kati ya 283) wafanyakazi wa majumbani waliripoti kupokea msaada wa chakula kutoka kwa serikali. Ingawa kuna sera rasmi iliyotekelezwa. Inawezekana kwamba wahojiwa walitaja msaada wa chakula uliotolewa na mashirika mengine.

# Afya na Usalama


Ingawa wafanyakazi wa majumbani, na wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kwa ujumla, wanaweza kupata bima ya afya kupitia moja ya mifuko ya hifadhi ya jamii ya malipo ya kabla (haswa, Mfuko wa Afya ya Jamii na Tiba Kwa Kadi), bado wigo ni mdogo sana. Kati ya wafanyakazi wasio rasmi, chini ya 5% kwa sasa wana bima ya afya (Verburgge et al, 2018).

Baadhi ya waliohojiwa walionyesha hofu ya kuugua, na kwa wafanyakazi wanaoishi na waajiri wao walionyesha hofu ya kufa wakiwa mbali na familia zao na kutopata mazishi sahihi. Hofu ya kuugua pia inaonekana katika matumizi ya vifaa vya kujikinga: wafanyakazi wote wa majumbani ambao waliendelea kufanya kazi mnamo Julai walitumia aina fulani ya vifaa vya kinga, kati yao barakoa (100%), dawa ya kusafisha mikono (73%) na sabuni (74%) zilikuwa za kawaida.

Kati ya kaya sita ambazo zilipata dalili za ugonjwa wa COVID-19 au ugonjwa wenyewe, watatu walipoteza wana familia na wanne hawakutafuta  huduma za afya. Sababu kuu zilikuwa wasiwasi juu ya kuambukizwa au kutengwa kwenye vituo vya matibabu na ukosefu wa uaminifu na ubora wa watoa huduma za afya.



**2%** (kati ya 283) ya wafanyakazi wa majumbani walipata dalili au ugonjwa wa COVID.



**100%** (kati ya 244) ya washiriki ambao walifanya kazi mnamo Julai walitumia aina fulani ya vifaa vya kinga.



**89%** (kati ya 216) ya wahojiwa walipokea vifaa kinga kutoka kwa mwajiri wao.



*“Mfanyakazi asiyeishi na mwajiri, anachukuliwa kama mtu ambaye anaweza kuwa mbebaji wa virusi. Wanalazimishwa kubadilisha nguo zao, kuvaa barakoa, kutumia vitakasa mikono, kunawa mikono. Maelekezo yote haya yalitolewa kwao katika kipindi hiki cha Covid. Kwa wanaoishi na waajirii, hawatakiwi kwenda nje ili kupunguza uwezekano wa kuugua. Wanatakiwa kukaa nyumbani kila wakati. “*

**- Kiongozi wa wafanyakazi wa majumbani**




*Zanini Athumani ni mfanyakazi wa majumbani mwenye umri wa miaka 40 ambaye anategemewa na watoto pamoja na wazazi. Picha na: Fanuel Halelwa.*

# Wasiwasi katika Kaya

**Huduma na majukumu mengine ya nyumbani/kaya**

Wafanyakazi wa majumbani wanaoishi na waajiri wao waliripoti mabadiliko makubwa katika utunzaji na majukumu mengine ya nyumbani wakati wa kipindi cha janga. Takriban robo yao waliripoti kuongezeka kwa shughuli zinazohusiana na kupika, kufanya usafi au utunzaji wa watoto na wagonjwa. Kwa kuongezea, 27% ya wafanyakazi wanaoishi na waajiri walifanya kazi masaa mengi katika kipindi hiki (asilimia kubwa kuliko wafanyakazi wasioishi na waajiri).

**% ya wafanyakazi wanaoripoti ongezeko la utunzaji na majukumu ya kaya-waishio na mwajiri**




Kumbuka: Ukubwa wa sampuli hutofautiana katika shughuli kwa sababu ya kukosa data za wafanyakazi wanaoishi kwa waajiri wao. Kwa shughuli iliyopewa, sehemu ya wahojiwa wanaoripoti ongezeko huhesabiwa nje ya idadi ya watu na data isiyopotea.



*"Wafanyakazi wa majumbani hapa nchini hufanya kila kazi mahali pa kazi. Yeye hufanya kazi za kufua, kutunza watoto na kupika. Yeye ni kila kitu; anafanya kila kazi. Kazi ambayo inaweza kufanywa na watu wawili au watatu inafanywa na mmoja... maadamu wewe ni mfanyakazi wa majumbani, basi lazima ufanye kila kazi nyumbani kwa mwajiri ".*

**- Said Wamba, Katibu Mkuu wa CHODAWU**



*"Hali nyingine kwa wafanyakazi wa majumbani wanaoishi na waajiri ni kwamba wanakosa uhuru kwa sababu wakati mwingine hawawezi hata kufanya ibada na angalau kujifunza jinsi mambo yanavyokwenda nje, au kuhudhuria semina. Wanazuiliwa sana, hawana uhuru. "*

**- Kiongozi wa Wafanyakazi wa Majumbani**

# Hatua za usaidizi

### Serikali

Hakuna hatua za misaada za COVID-19 zilizotekelezwa nchini Tanzania. Hivi sasa serikali imejikita katika kutoa misaada ya kiufundi kwa wafanyakazi wa afya (miongozo juu ya usimamizi wa janga la corona, kuzuia na kudhibiti maambukizo mnamo Aprili na Mei) na kutambua vituo vya kujitenga; pia imetangaza mpango wa kufungua sekta ya elimu na kutekeleza sera kulinda usalama wa sekta ya fedha.

**0%** ya wafanyikazi wa majumbani walipokea misaada ya kifedha kutoka kwa serikali.


**16%** 16% ya wafanyakazi wa majumbani walipata msaada wa chakula.

### Mashirika ya ndani ya Wafanyikazi wa sekta isiyo rasmi.

Bila msaada maalum (kifedha au kijamii) kwa wafanyakazi wa majumbani, vyama vya wafanyakazi vilichukua jukumu muhimu. Jijini Dar es Salaam, wafanyakazi wa majumbani 128 walipokea msaada wa chakula kutoka CHODAWU. Mbali na msaada wa chakula, chama kilitoa elimu ya utambuzi kupitia kampeni za uhamasishaji. Kwa kupitia redio na Televisheni wafanyakazi wa majumbani waliweza kupata ujumbe uliolenga msisitizo juu ya hatua za kinga na wito kwa waajiri kutowabagua au kuwanyanyapaa wafanyakazi wa majumbani.

Kati ya wafanyakazi waliohojiwa, 98% walipokea habari juu ya jinsi ya kujikinga na COVID-19, haswa kutoka redio na Runinga, waajiri wao, na chama chao cha wafanyakazi.

**% Ya wafanyakazi waliopokea habari ya COVID-19 kutoka ...**




*"Serikali ilitoa elimu na kuongeza uelewa. Kila manispaa watu walizunguka kujenga uelewa, Ukienda kila nyumba kulikuwa na ndoo ya maji na sabuni. Sikuwa nimewahi kuona hii maishani mwangu. Iwe nyumbani,madukani katika sekta isiyo rasmi na masoko. Kila soko lilikuwa na ndoo ya maji. Huu ulikuwa ubunifu mkubwa na uelewa. "*

**–Vicky Kanyoka, Mratibu wa Mkoa wa IDWF Afrika**

5 16% (kati ya 283) wafanyakazi wa majumbani waliripoti kupokea msaada wa chakula kutoka kwa serikali. Ingawa kuna sera rasmi iliyotekelezwa. Inawezekana kwamba wahojiwa walitaja msaada wa chakula uliotolewa na mashirika mengine.

# Mikakati ya Kukabiliana na Marekebisho

Bila msaada kutoka kwa serikali, wafanyakazi wa majumbani wanageukia mikakati mingine ya kukabiliana na Janga. Wengine wamegeukia aina zingine za kazi, kama vile kufua, kupika na kuuza vitu (k.m matunda, nguo za mitumba, pipi). Kati ya wale waliopoteza kazi zao mnamo Aprili, theluthi mbili wametafuta msaada wa kifedha kutoka kwa wanafamilia.



**54%**


Ili kukabiliana matokeo ya janga hilo, 54% ya wafanyakazi wote wa majumbani walitumia angalau moja ya mikakati ifuatayo:

- kukopa fedha
- kutumia akiba au kutafuta msaada kutoka kwa familia,
- marafiki au majirani

Kati ya wale waliopoteza kazi mwezi Aprili, **84%** walitumia mikakati kama hiyo ili kukabiliana na janga hilo.

Kwa kushangaza, 36% ya washiriki wote waliripoti kutumia akiba yao, uenda kwa sababu ya kupoteza kipato au kuongezeka kwa gharama za maisha, hasa chakula. Ingawa ni muhimu kwa uhai wa muda mfupi, vitendo hivi vitakuwa na athari mbaya kwa uthabiti wa wafanyakazi na uwezo wa kama kabla ya janga.

**Mikakati ya kukabiliana**






*Maisha yalikuwa magumu sana, nilifanya uamuzi wa kurudi kijijini"*
**Mfanyakazi wa Nyumbani Mwanamke**

# Matarajio ya kurudi katika hali ya awali

### Mahitaji ya Wafanyakazi wa Majumbani

Wafanyakazi wengi wa majumbani walioshiriki katika utafiti huu walisisitiza hitaji la mishahara bora na mikataba ya ajira, pamoja na bima ya afya, likizo ya kila mwaka na usalama wa kijamii. Kama Kielelezo cha mishahara yao midogo na kuongezeka kwa gharama za maisha zilizosababishwa na janga hilo, wafanyikazi wengi pia walizungumza juu ya hitaji la kupokea msaada wa kufidia usafiri na chakula.

Viongozi wa kisekta walielezea hali ambayo wafanyakazi wa majumbani hawatendewi kama wafanyakazi wengine, kama ilivyo kwa wafanyakazi wa serikali, na hitaji la kujenga usawa kati ya makundi haya mawili.

### Mpango Bora kwa Wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi

Maeneo muhimu ya msaada katika ngazi ya kitaifa ni pamoja na:

- Kuridhia Mkataba wa ILO Na. 189 kwa wafanyakazi wa majumbani na mifumo bora ya utekelezaji wa sheria iliyopo ya kitaifa inayodhibiti hali zao za kazi.
- Kuboresha uhusiano wa ajira, pamoja na mikataba ya ajira ya maandishi inayoeleweka.
- Njia maalum za kuwalinda wafanyakazi wa majumbani wanaoishi na waajiri wao pamoja na wafanyakazi wahamiaji.

# Marejeo

Government of United Republic of Tanzania. 2014. *Integrated Labour Force Survey. Analytical Report 2014*, Dar es Salaam.

International Labour Organization (ILO). 2016. *A Situational Analysis of Domestic Workers in the United Republic of Tanzania*. Dar es Salaam, ILO.

Verbrugge, Boris, Adeline Ajuaye, and Jan Van Ongevalle. 2018. *Contributory Social Protection for the Informal Economy? Insights from Community-Based Health Insurance (CBHI) in Senegal and Tanzania*. Belgium, BeFind.



*Mariam Sadiki ni mfanyakazi wa majumbani mwenye umri wa miaka 25 ambaye anategemewa na wazazi. Picha na: Fanuel Halelwa.*

**Janga la COVID-19 na Utafiti  wa uchumi usio rasmi** ni ushirikiano kati ya mtandao wa kimataifa wa Wanawake katika sekta ya Uchumi usio Rasmi: Utandawazi na Ushirikiano (WIEGO) na mashirika washirika wa ndani wanaowakilisha wafanyakazi wa sekta isio rasmi katika miji 12: Accra, Ghana; Ahmedabad, India; Bangkok, Thailand; Dakar, Senegal; Dar es Salaam, Tanzania; Delhi, India; Durban, Afrika Kusini; Lima, Peru; Jiji la Mexico, Mexico; Pleven, Bulgaria; New York City, USA; na Tiruppur, India; kwa msaada kutoka Kituo cha Utafiti wa Maendeleo ya Kimataifa (IDRC / CRDI), Canada. Utafiti uliochanganywa wa njia ndefu ni pamoja na dodoso za uchunguzi wa wafanyakazi wa sekta isio rasmi na mahojiano yaliyopangwa na viongozi wa wafanyakazi wa sekta isio rasmi na watoa taarifa wengine muhimu, yote yalifanywa kwa njia ya simu. Mzunguko wa 2 utafanyika Machi na Aprili 2021. Kwa habari zaidi, tembelea wiego.org/COVID-19-Global-Impact-Study.

Wanawake katika Ajira Isiyo Rasmi, Utandawazi na Uhamasishaji (WIEGO) ni mtandao wa ulimwengu unaolenga kuwawezesha wanyonge wanaofanya kazi, haswa wanawake, katika uchumi usio rasmi ili kupata maisha yao. Tunaamini wafanyikazi wote wanapaswa kuwa na fursa sawa za kiuchumi, haki, ulinzi na sauti. WIEGO inakuza mabadiliko kwa kuboresha takwimu na kupanua maarifa juu ya uchumi usio rasmi, kujenga mitandao na uwezo kati ya mashirika ya wafanyikazi wasio rasmi na, kwa pamoja na mitandao na mashirika, kuathiri sera za kitaifa, kitaifa na kimataifa. Tembelea www.wiego.org.

**CHODAWU**, Chama cha Wafanyakazi wa Hifadhi, Hoteli, Majumba, Huduma za Jamii na Ushauri, kimekua kikifanya kazi katika kutetea wafanyikazi wa nyumbani na sekta zingine tangu 1996. Chama hicho kinatoa mafunzo na ushauri nasaha na hutoa msaada wa kisheria kumaliza migogoro na waajiri; pia kjinafanya kazi ya kukuza uelewa kati ya wafanyikazi wa majumbani na waajiri juu ya haki zao. CHODAWU kwa sasa inatetea kupitishwa / kuridhiwa kwa Tanzania kwa Mkataba wa Wafanyakazi wa majumbanina 189.

WIEGO
Women in Informal Employment: Globalizing and Organizing

CHODAWU

Kazi hii imefanywa kwa msaada wa ruzuku kutoka **Kituo cha Kimataifa cha kukuza maendeleo ya kumbukumbu -** Ottawa, Canada.  (**International Development  Research Centre,** Ottawa, Canada) maoni haya yaliyotolewa hapa sio lazima yawakilishe yale ya Kituo cha Kimataifa cha kukuza maendeleo ya kumbukumbu (IDRC) au Baraza lake la Magavana.

IDRC | CRDI
International Development Research Centre
Centre de recherches pour le développement international

Canada